

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

*Anwani ya Simu: "REGCOM"
Simu ya mdomo: (028) 2220215-18
E-mail: ras.kagera@pmoralg.go.tz
Fax: (028) 2222341 / 2221356
Tovuti: www.kagera.go.tz*



**OFISI YA MKUU WA MKOA,
S. L. P. 299,
BUKOBA - KAGERA.
TANZANIA.**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI
TAREHE 03 AGOSTI, 2019**

Ndugu Waandishi, Nimewaiteni hapa kwa lengo kuu moja la ushiriki wenu katika Wiki ya Uwekezaji Kagera lakini pia kupitia kwenu na vyombo vyenu vya habari vilivyopo ndani na nje ya mkoa nitumie fursa hii kuwaalika wadau mbalimbali wa uwekezaji pamoja wananchi wote nje na ndani ya mkoa kushiriki katika Wiki hiyo ili kujionea fursa mbalimbali zinazopatikana katika mkoa wa Kagera. Mgeni Rasmi katika Wiki ya Uwekezaji Kagera atakuwa Waziri Mkoo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb).

Ndugu Waandishi, Wiki ya Uwekezaji Kagera inatarajia kuanza Agosti 12 hadi 17, 2019. Wiki ya Kagera itaanza na maonesho ya bidhaa au fursa mbalimbali zinazopatikana katika mkoa wa Kagera tarehe 12-13/08/2019 na maonesho hayo yatafanyika katika viwanja vya Gymkhana Manispaa ya Bukoba.

Aidha, tarehe 14/08/2019 Wiki ya Kagera itafunguliwa rasmi na Mgeni Rasmi Waziri Mkoo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa kufungua rasmi Kongamano la Wadau wa Uwekezaji litakalofanyika katika ukumbi wa Hoteli ya ELCT Bukoba kuanzia saa 3:00 asubuhi.

Ndugu Waandishi, Tarehe 15 Agosti, 2019 Kongamano la Wadau wa Uwekezaji litaendelea ikiwa ni pamoja na maonesho katika viwanja vya Gymkhana. Tarehe 16/08/2019 Wiki ya Uwekezaji Kagera inatarajiwa kufungwa rasmi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkoo Uwekezaji Mhe. Angela Kairuki, lakini mara baada ya kufunga rasmi wadau mbalimbali wa uwekezaji watapata nafasi ya kwenda kutembelea vivutio mbaimbali vya utalii pamoja na fursa mbalimbali za uwekezaji zilizomo mkoani Kagera hadi tarehe 17/08/2019.

Ndugu Waandishi, Kauli Mbiu ya Wiki ya Uwekezaji Kagera ni "**Kagera: Eneo la Kimkakati kwa Uchumi Wetu na Afrika Mashariki.**" Kauli mbiu hii imelenga kuonesha mkoa wa Kagera ulivyo kitovu cha uchumi wa nchi za Afrika Mashariki na Kati katika kuyafikia masoko ya nchi hizo za Rwanda, Burundi, Uganda, Kenya, Sudani Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (DRC). Ambapo soko hilo lina wingi wa watu wasiopungua milioni 190 lakini pia soko la ndani ya mkoa na soko la mikoa iliyopo Kanda ya Ziwa ya Mwanza, Geita, Shinyanga pamoja na Kigoma.

Ndugu Waandishi, Wiki ya Uwekezaji Kagera ni fursa kwa wadau mbalimbali wa uwekezaji kuja hapa kwetu kuwekeza hasa katika sekta za Kilimo kutokana na misimu miwili ya mvua kwa mwaka lakini pia mazao mengi ya chakula na biashara yanakubali sana katika mkoa wa Kagera mfano Ndizi, Kahawa, Vanilla, chia, kokoa na mazao ya chakula ni mahindi na mahage. Fursa nyingine ni uvuvi, ufugaji, Viwanda, Elimu, Utalii na Utamaduni wa wananchi wa Bukoba.

Ndugu Waandishi, Wito, Kwanza nitoe wito kwenu Waandishi wa Habari, Wahariri, Wamiliki wa Vyombo vya Habari pamoja na wadau wote wa habari kuanzia sasa kwa pamoja kwa nguvu moja tuitangaze Wiki ya Uwekezaji Kagera sisi kama wadau muhimu wa ndani ya mkoa ili kuwahamasisha wananchi wote ndani na nje ya mkoa kuja na kushiriki kikamilifu katika wiki hiyo ili tuufungue mkoa wetu kimtaji na kiuchumi na kutengeneza ajira za vijana wetu.

Pili, nitoe wito kwa taasisi zote za Serikali na zisizokuwa za Serikali zilizopo hapa mkoani Kagera kuhakikisha zinashiriki kikamilifu katika Wiki ya Uwekezaji Kagera ili kuonesha fursa walizonazo na kujitangaza kwa wadau mbalimbali ambao tunawatarajia kuhudhuria katika wiki hiyo kutoka ndani na nje ya nchi.

Ndugu Waandishi, Namalizia kwa kusema kuwa "**Kagera: ni Eneo la Kimkakati kwa Uchumi Wetu na Afrika Mashariki.**" Ni wajibu wetu sote Wanakagera kushiriki katika Wiki ya Kagera ili kuinua uchumi wa Mkoa wetu kwa kuchangamkia fursa mbalimbali za Kagera.

Imetolewa na; Brigedia Jenerali Marco E. Gagut
Mkuu wa Mkoa
KAGERA